

## **CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**VERBATIM REPORT OF**

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, IGEMBE  
CONSTITUENCY AT MAUA GIRLS SECONDARY SCHOOL HALL**

**ON**

**OCTOBER 10<sup>th</sup> 2002.**

**RECORDS OF PROCEEDINGS DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL IGEMBE  
CONSTITUENCY MAUA GIRLS SECONDARY SCHOOL HALL, OCTOBER 10<sup>th</sup> 2002.**

**Present.**

1. Com.Domiziano Ratanya.

## Secretarial Staff in Attendance.

1. Solomon Anampiu	Programme Officer
2. George Kimathi	District Cordinator
3. Mary Babu	Verbatim Recorder

Meeting started at 10.00 a.m with Com. Ratanya as the chair.

**George Kimathi:** I think we have to start, because I can see people are coming and leaving. Those who are there we start then others will find (inaudible) watakujbaadaye. **Kama** mjuavyo ni kwamba leo tuko hapa Maua Girls kwa sababu ya launching ya Draft Constitution. Tuko na Commissioner from the headquaters, we have a programme officer, these are the people ambao watatuongoza katika hiyo Draft Constitution, na kisha tutna coordinator lakini ningetaka kurudia kidogo hapo. Kwanza mwenyewe nimekuja hapa kama mara tatu hivi, na nina programme officer bwana Solomon Anampio ambaye ametoka office yetu, na mwagine ni Mary Babu na ni officer kutoka kwa office yetu ambaye anaangalia mambo ya verbatim recording. Mimi wale ambao hatujakutana nanyi mimi naitwa ndugu Domiziano Ntochokera Ratanya. Mimi nimekuja hapa hata nimeenda Ntonyiri wakati mwagine nikaenda area zote area hii, na hata hapa kwenyewe, especially wakati tulianza civic education na sasa tuko hapa na ninyi.

Kitu cha kwanza, wale wameingia ningetaka kutoka wakati huu niseme ya kwamba tumeanza mkutano wa Constitutional with Kenya review Commission hapa katika Igembe Constituency. Kwa hivyo kutoka sasa mpaka tumalize, mjisikie ya kwamba mna uhuru wa kusema lolote hapa, kwa sababu mkutano wetu una security ya kutosha kwa kisheria, kwa hivyo unaweza kusema lolote, unaweza kuuliza lolote bila kuogopa. Siku ya leo ningetaka mjue ni kitu gani mnakuja kufanya, siku zingine zote ilikuwa kazi tofauti, lakini ya leo ni ingine nayo katika kazi yetu ya Commission. Hii nikuwaletea hii tunaita Draft Bill ya Constitution. Hii tunaita launching yaani kuanza, na kuwaambia tumeanza kuisoma na kujadiliana mpaka kutakuwa na mkutano wa wajumbe ambao umechagua delegate wenu ambao watakutana Nairobi. Hii si ndio siku tuli-launch yaani kuanza? Lakini hii ni siku ya kuja kwa Constituency.

Nikiangalia katika hii Draft pengine wale wamepewa wale wamepata nafasi, kupata tuan zingine kidogo. Tarehe ishirini na saba mwezi wa September ndio tulianza hii na tukawapatia WanaKenya wote katika magazeti, wanasikia kutoka kwa radio, na njia nyingine zote waendelee na kujadiliana hii report ya Constitution ambayo tumeifanya proposal ambayo itakuwa Constitution baadaye. Tulianza tarehe ishirini na saba mwezi wa tisa, ukihesabu hiyo siku kutoka 27<sup>th</sup> mwezi mmoja ama thirty days itakuwa 27<sup>th</sup> October na sheria inasema kwamba, hii tui-publish tupatitie wananchi waendelee kujadiliana kwa siku thelethani for thirty days. Ikifika siku hiyo thelathini lazima tuwe na national conference.

Na National Conference mkutano utakuwa Nairobi, wa delegates wote wamechaguliwa kulingana na sheria yetu, ambao

watakutana huko na tunaona namba itakuwa six hundred. Hapa mna watatu na hata kutoka makanisa na groups zingine, lakini wale watatu ni wa district. Tuna mama mmoja ambaye anawakilisha kutoka district na unajua akiwa delegate, si akina mama peke yake ana akilisha ana akilisha kina mama na kila mtu. She is a full delegate na wengine wawili. I(inaudible) whether they are here, you could also introduce them but the lady is here. Kwa hivyo hawa watatu ni wa district na kuna wengine wametoka vikundi vingine kama vya akina mama, kama makanisa na political parties, hawa watu wote watakutana Nairobi on 28<sup>th</sup> October.

Kwa hivyo kutoka sasa tumewaletea hii muisome, ni kwamba kulingana na hii sheria inatusimamia katika sheria hii ya Commission inaitwa Cap 3 laws of Kenya. Inasema kulingana na vile tulibadilisha kidogo, inasemekana tusome kwa siku thelathini halafu tuwe na conference. Wakati tunapoanza hii katika Igembe Constituency na Commissioner wako round kila pahali, wako Mombasa, wako Kisumu, wako huko Embu, tunazunguka Constituency zote 210.

Mpangilio wa leo ambao ningetaka kuwaeleza vile tutaendelea kutoka sasa, kwanza tumefanya hiyo tunaita introduction. Nimewaambia ile kazi ambayo tunakuja kufanya na kuweza kuwaeleza zaidi ile kazi tutafanya. Kwanza tutazungumza mambo ya report ambayo Commission ilifanya huko Mombasa tarehe kumi na nane ika-launch, short report, ambayo tulifanya tarehe kumi na nane mwezi wa tisa. Tutazungumza hiyo kwa dakika chache. Halafu tukimaliza hiyo, tutaingia kwa hii, tutazungumzia hii na kuona jinsi ya kuisoma. Ili mjue vile mtaendelea.

Tukimaliza hayo sasa mimi nitasimama hapo nitawapatie nafasi mtu aulize na pengine yale maswali ambayo utauliza yatatokana na yale ambayo mmesoma hapa, ama yale mmesikia kutoka kwa mimi ama kwa officers wengine hapa. Na usiende nje ya yale ambayo tunayo, nasikia kwamba tulianza stage ya civic education tukaenda ya hearing, hizo zote. Hearing yenyewe tulimaliza, kwa kuja kwa Katiba ama kutengeneza hii Draft ya Katiba tumewaletea maoni yako hapa. Hii file ni ya Igembe Constituency. Ukiangalia hapo utaona summary ya yale mlisema siku ile Commissioners walikuja hapa. Yale maneno yote mlisema, infact nilikuwa hapa wakati wa hearing, tulikuwa hapa na Commissioner mwingine anaitwa Abubakar. Yale tulichukua yamewekwa na staff wetu yakaandikwa vizuri, yakapangwa, ndio yako kwa hii file. Hiyo ilikuwa wakati huo kupeana maoni.

Siku ya leo si kupeana maoni, ni kuwaambia yale ambayo mltuambia tumeyaweka kwa language ya Constitution yenyewe ambayo ikijadiliwa kutoka sasa baadaye itakuwa Constitution na ikienda through the Parliament hiyo stage imebaki itakuwa Constitution. Kwa hivyo kama hukuja siku ile tulipatiwa mambo yenu hapa malalamiko, siku ya leo si ya kuleta maoni. Yale maswali utauliza ni maswali inahusu hii Draft tumetengeneza ili tusirudi huko nyuma. Kwa hivyo wakati mnauliza maoni yenu queries na nini, muwe mnajua ya kwamba sasa ile inaitwa report sasa ya Katiba. Hatuko kwa ile stage ya malalamiko au views, hiyo tulipeana. Sasa tuko stage ya mswanda ambao utakuwa ni Katiba.

Kwa hivyo nitaanza kwa report kwanza: hii report tunaita short version au report fupi. Hatukuweza kuwa na copies za kupatia kila mtu kwa sababu ilitoka tarehe kumi na nane mwezi wa tisa tukiwa Mombasa. Wakati tulipoendelea na kuona mambo yenu

yote na katika 210 constituencies tilitoka na ripoti short, na hata hii ilienda kwa magazeti, lakini siku ya leo ile copy tunayo iko inform of this book na programme coordinator alikuwa na copy chache ambazo sitakuwa kwa documentation center. Sasa kwa hii yenyewe yale kwa hii, hii si Constitutional yenyewe au Draft yenyewe, hii ni ripoti ya kuonyesha vile kazi tuliendelea kuifanya na pale tumefika.

Kwanza kwa hii report inaeleza background ama mwanzo wetu tulianza kwa hii report wakati mtakuwa mkisoma, mtaona hata kuna list ya Commissioners. Commissioner wetu ni 27 na Commissioners wawili ambao tunaowaita ex-official. Mmoja ni Attorney General, yule mkuu wa sheria na mwininge ni secretary wetu Lumumba. Hao ni ex-officials lakini (inaudible) ambao walichaguliwa kama Commissioners, na hawa wengine ni wafanyi kazi wetu amba wanatusaidia. Kama Attorney General ni legal adviser na tena ni Attorney General wa Serikali, secretary wetu naye ni mipango yote ya secretariat na kila kitu anatufanya. Kwa hivyo timu yote we are 29. Utaona kwa hii report mambo kama hayo yako. Lakini majina yetu na mambo kama haya hayako kwa Draft. Hii ni Draft ambayo itakuwa Constitution na Constitution haiwezi kuwekwa mambo mageni. Ni yale tu proposal ya yale mnataka yawe katika nchi yetu na vile nchi itaendeshwa. Kwa hii report tena, mkiendelea kuangalia hii report mtaona vile tuliendelea na kazi yetu, ile process iliendelea na vile it goes na values. Mtaona ya kwamba kwanza tulianza na civic education, tukawafundisha watu Katiba hii ambayo tunaendelea kutengeneza mpaka wakaelezwa ni kitu gani na itakuwa na mambo gani, hiyo kazi ikaisha na kutoka hapo tukaenda kwa mambo ya kuchukua maoni ya wananchi, tukaenda what we call listening to the people, tukaenda kwa kila Constituency tukisikia maoni ya wananchi. Hiyo stage nayo tukaenda round kwa miezi sijui kama mitatu hayo mambo yote tukamaliza.

Kwa huuwakati unasoma utaona kuna picha zingine kama hapa, we are all Kenyans. Kwa hivyo hii Katiba inatengenezwa na Kenyans yaani ni ya wananchi. Ukiendelea kwa hii report utaona kwamba Commissioners walichukua hizi hearings zote, maoni yote haya yote. Hii ya Igembe iko hapo, ya Ntonyiri, Tigania, Imenti, pahali pote 210 constituencies kama hii tukaichukua tukaenda kuketi huko Mombasa, tukaizungumzia tukazungumza mpaka tukakubaliana haya yote tutaweka kwa Draft Constitution. Kwa hii report sitaendelea kusoma yote kwa sababu siku ya leo niliwaambia si mimi nitakuja kusoma lakini tu-give highlight kuonyesha pale ile step tuko. Tutaendelea kusoma muone maoni yale yamewekwa kama summary form. For example tukienda kwa hii page one hapa, how is the new Constitution different from the old?

Nitaangalia hii Constitution ambayo tuna-change kama tukisoma pahali pamoja hapo kwa mfano. It reflects what people are concerned about instead of being mainly a set of fundamental structures. Hii ni kwa sababu ni people driven ina yale mambo wenye wamesema, watu wa Kenya. Pengine kitu kimoja hapa kinaweza kusemwa na watu ishirini, hatuvezi kuandika hayo yote, lakini tutaandika summary hao watu walisema. Kuna point moja nyingine inasema a person doesn't have to be a member of a party in order to stand for elections. Katika Draft yetu mpya utaona tofauti moja ni hii.

Kwa sasa current Constitution niliweza kuja na copy yangu ya current Constitution ambayo tuko nayo katika siku ya leo. Hii iko sasa hii, ni law ya current Constitution ambayo tunayo. Utaona kwamba, ukiangalia kwa hii lazima uwe sponsored by the

party katika old Constitution lakini hii Draft ikiwa sheria iko Constitution mtaangalia hata ndani mtaona yale tume-recommend hakutakuwa na sababu uwe nominated by the party kama huna party. Kama kila mtu ana party. Kuna wengine hawana party na anataka kuwa kiongozi. Kwa hivyo new Draft we have recommended something ile zamani tulikuwa tuanita independent candidate.

Wale wameishi miaka mingi kidogo wazee kama mimi, mnajua kwamba kulikuwa na independent candidates zamani. Kulikuwa na mtu alikuwa analetwa na party hii au nyingine, na tena kuna mtu ambaye hana party yoyote. Kwa hivyo yeye anaweza kuwa kiongozi, kwa hivyo alikuwa na nafasi ya kupigiwa kura na wananchi. Kwa hivyo hata sasa kutakuwa na hiyo nafasi. Ndio unaona difference hii moja nimesoma, a person doesn't have to be a member of a party in order to stand for election. You can stand for election even if you are not a member of any particular party, even if you are not a member of DP, KANU, SDP, whatever you can stand for election as an independent candidate as per new Constitution wakati utakapomaliza kazi yake in the Constitution. unaweza kuingia namna hiyo.

Then, ni mfano tu natoa kwa hii report kwa sababu sasa tutaacha muendelee kusoma, sitaendelea kuwasomea yote lakini ni njia ya kusoma. Kitu kimoja hapa, point ningetaka kusoma hapa. There will be a leadership code Governing the behaviour of the MPs and the other leaders and the machinery for enforcing its principles. Kuna njia moja ya muhimu itakuwa hapa sasa kwa Katiba hii mpya, kama MP mnaona hafanyi kazi, hamuwezi kukaa na yeye miaka mitano. Mkiwa hamtaki ama mnaona hafanyi kazi. Leo kuna machinery ama kuna njia katika Katiba hiyo mpya ambayo itatoka, kumuondoa huyo MP na pengine mchagua mwengine. Vile vile kuna njia ya kuondoa President na mwengine awekwe. Lakini kwa hii ya sasa haya mambo hayako. Haya ni mambo mengine. Kuweza kumuondoa mpingwa huu tunaye leo, itakuwa ni mambo magumu utaona atangoja karibu miaka hiyo tano ama yote kwa kuwa pengine alisign. Lakini kwa new Constitution kuna njia imekubaliwa na Katiba ambayo unaweza kutumia, hiyo tutaona kwa Draft, kutumia kumuondoa MP, should be recalled aende nyumbani na muweke mwengine.

Nikisoma part ingine hapa, administration police are to change their separate identity. Administration police wetu ambao tunao sasa askari wetu wataingia polisi wote watakuwa ni askari ya polisi. Hata hiyo ni tofauti hakuna mtu ambaye atapoteza kazi yake. Mnaona hata ingiya tutakuwa na new Constitution si kusema ati kama Ratanya atageuka awe mweupe awe na mna gani, si tutaangalia vile tulivyo? Ni mageuko tu kidogo ya ufanyi kazi, hakuna kitu sana ambao kinachukiza sana, ni kugeuza mambo kidogo kidogo. Wote watakuwa ni askari wa polisi wote watakuwa kikosi kimoja. Hiyo ni mbaya. Watu wengi walikuwa wanasema hata nikipata nafasi ya kusoma nitasoma, utasoma juu nitaacha hii. Utaona hata ninyi pengine mlisema hivyo.

Hayo ni mambo ambayo tulisikia kwa kila Constituency, si mambo ya Commissioners, tuliweka pamoja tukasema wananchi wengi wanasema hii polisi mbili ni ya nini? Si tuweke polisi wawe kitu moja. Kwa hivyo Katiba mpya utaona hayo mambo yatakuwako, okay? Kuna point ingine utaona itakuwa tofauti kidogo. The President can be removed from office by a process of impeachment at the instance of Parliament. President anaweza kuondolewa kwa hii njia tunaitwa impeachment. Yaani unafanyiwa procedure ya kumuondoa kama ni investigation, kumfanyia kesi fulani hivi, mpaka itaonekana kama atapatikana

namakosa, anaondoka halafu mnaenda kwa debe tena kuleta mwengine. Kwa hivyo kwa hii Katiba hiyo mambo itakuwako. Na nilisema iwe impeachment namna hiyo.

Inginge mataona tutakuwa na tofauti kidogo na hii ya zamani, there will be a new supreme court at the end of the judicial system, (inaudible) all new judges or new even ni wale wako wapatiwe kazi mpya. Sikusema ya kwamba kuna mtu atafutwa lakini, lakini yule anafaa atakuwa huko tu. Yule ambaye wakati wake mwengine umefika pengine wengine atakuta hayuko, ama yule ataonekana si lazima aweko. Si kusema kuna watu watadhuluiwa, ni change.

Tulikuwa kwanza up to the court of appeal, kutoka magistrate, ama hapa mko na magistrate court na Maua hapa nasikia kuna stage ya senior magistrate. Kuna mahali pengine kuna magistrate ambaye ako chini kidogo. Sasa kutoka kwa magistrate mpaka kwenda kwa court of appeal, lakini Katiba hii itatoka, tumependekeza kuwe na court ingine juu ya court of appeal. Ukiona hutosheki kwa court of appeal unaenda kwa supreme court. Hiyo imewekwa na hiyo ni tofauti na hii Katiba tunayo sasa. Na hata tumependekeza ya kwamba kutakuwa na village tribunals, kutakuwa na court huko kwa village huko nyumbani. Ma case mengine yale ambayo yakienda kortini yanakaa miaka mingi yatakuwa yanatatuliwa na wazee katika korti ambazo zitafanywa that is the grassroot. Na yale hayatawezekana yataenda juu kidogo pengine kwa location, kwa district magistrate, district magistrate ako mpaka highcourt, the court of appeal, mpaka supreme court. Kwa hivyo utaona kwa hii Draft kuna hiyo maelezo na kuna hiyo change.

One more thing is that, ingine ningetaka muangalie ni Ministers will be appointed outside of Parliament. Once they are appointed they will become ex-official members of Parliament, hio dio tofauti itakuwa kubwa sana. Sasa Minister atakuwa kama yule mjambe ambaye amechaguliwa, anaenda amechaguliwa na anapewa pendera yake, si amekuwa Minister na the same time ni MP wa area na tena ni Minister wa Government sasa. Lakini kwa hii Draft itakuwa Constitution tumependekeza Ministers wachaguliwe outside, yaanij wasiwe MPs, in that case watakuwa ex- officials of Parliament. Yaani ni kwamba watakuwa wanaketi kwa Parliament kujibu maswali ya ministries.

Kama ni ministry of education, kutakuwa na Minister of education ambaye amechaguliwa na Bunge, ama ministry of health, na cha muhimu ni kwamba hawa Ministers lazima awe anajua hiyo kazi. Si kutoa daktari aende kuwa Minister for law. Minister for law awe amefanya hiyo degree ama hiyo course. Kama ni health awe pengine amekuwa daktari na awe na qualification of doctor yote. Wengine Parliament akisema ni lazima awe kiwango ya PHD ile ya juu zaidi au hata anajua kuchinja huyo ndiye sawasawa pengine, ama namna gani? Ama manataka clinical officer awe Minister? (laughters) okay hiyo ni mfano tu ninawapatia. Lazima awe qualified na awe anaweza kusimamia hiyo ministry akiwa ni professional.

Mmekuwa na malalamiko mingi, unaskia Minister of education hajui njia ya kuingia class room ni wapi na unaskia ya kwamba ni education. Sasa huyo pengine education atakuwa ana degree ya education ya juu zaidi, na pengine wakitaka kuweka kwa njia sawa kabisa, wachunguze waone huyo mtu amefundisha at a certain level, hata kama amefundisha secondary school or

primary or university lakini awe na kiwango ya juu, lakini amekuwa a class room teacher somewhere hata akiwa professor na ana chokaa na anafundisha huyo ni classroom teacher. Si kusema ni mwalimu wa hapa classroom teacher peke yake, hata professor lakini awe amefundisha a certain level hiyo inaweza kuwa namna hiyo tu. Kwa hivyo akisikia ya waalimu, watoto, watoto atajua ni kitu gani hii tunasemaea. Asiwe pengine ni vitabu peke yake anasoma lakini anajua system.

Mtu wa agriculture awe amekuwa professional kwa agriculture na awe na qualification ya agriculture. Lakini mambo hayo yote ninawaambia hatukuweka kwa Constitution namna hiyo ni sheria Parliament itafanya kwa kuchagua Ministers, huo ni mfano tu nilikuwa nikisema. Ni Parliament yenye itasema, yule tunataka awe Minister, awe nana hii namna hii waweke law, wataweka hiyo guideline kwa kuonyesha vile watachagua Ministers na tumependekeza kwa Katiba yetu, kusoma kwa Draft ni fifteen Ministers na fifteen deputy Ministers. Sisi tunawaita deputy Ministers not assistant Minister na si Commission imefanya hivyo ni kutokana na hawa na waambia maoni yenu.

Tumetoa maoni kwa Constituency kama hii Igembe hii ambayo iko hapa report ile mlisema siku ile nilikuja hapa iko hapa. Tumetoa kwa kila mahali na hiyo tukaona watu wengi wanasma Ministers wawe nje. Kama ni MP awe ni Mp wa hiyo Constituency ili awe na nafasi ya kuangalia mambo hiyo ya Constituency, yaani huko dani na hata huko kwa mkutano yenye ya Parliament. asiwe anachikilia mambo mengi ama asiwe anachukua pesa huko ya maendeleo anapeleka kwao na anaachia pahali pengine pa Kenya na Minister wa Kenya. Kama ni Minister wa Kenya, kama kuna mambo ya maendeleo si agawanye kila pahali kwa hivyo kumekuwa na hopeless kwa watu.

Unasema kama pengine ni Minister for education anaenda anatengeneza kwao peke yake ili aweze kura next time. Anasahau hiyo kazi ya ujumbe kwake, pengine anakosa kukaa kwao sana anakaa Nairobi ama anaenda kwa mkutano na mambo kama hayo. Nilisikia watu wata-recommend hawa Ministers wakiwa nje. Awe tu hii ni mambo ya report katika Draft yenye nitaona vile imeedingia kwa kila section. (inaudible) hayo mafupi nimewaambia mambo ya hii ripoti tulitoa tarehe kumi nane mwezi wa tisa na hata tukaweka kwa Nation. Watu wengi walinunua ile pull-out ilikuwa huko, ilikuwa na picha mingi na ilikuwa inaeleweka sana.

Sasa kutoka hiyo kwa stage ingine tukaendelea kuangalia mambo ya wananchi walisema na hata hii report yetu mpaka 27<sup>th</sup> of September tukawa na hii tunaita Draft bill ya Constitution. Hii sasa vile ilivyo imewekwa kulingana na language ya Katiba au lugha ya kuandika vitabu vyta sheria. Ili ikienda ikiangaliwa na Parliament, watatoa makosa, watapendekeza na pengine watafanya iwe act of Parliament yaani iwe Constitutional of law. Lakini kabla ya kwenda kwa Parliament, mnajua ya kwamba kabla ya ninyi kusoma nimewaambia leo muuanze kusoma for thirty days. Hii mtaisoma, mtaiangalia in every chapter, every section, kwa sisi tunaita articles, section A ya Draft yetu ya Constitution tunaita articles. Tutayaangalia kila kitu na mkiona kuna mambo mngetaka kuongeza ama mngetaka kuondoa hiyo ni maoni yenu kwa sababu hamuwezi kusoma kitu kila kucomment.

Kama mko group ya akina mama, ya vijana, ya wazee na wengine wote namna hiyo na hata individual organizations, Non Governmental organization msome mpaka muone mambo yale mnaweza kupendekeza.

Mkiona point fulani hapo ndani na mnaona haikuwekwa kwa njia nzuri, mtacomment na hayo mapendekezo mkitoa mtayaleta kwa Commission in writing. Kama ni section fulani tutaingia kuangalia sections zingine sasa hivi. Kama ni section fulani utasema hii section mtasema hii section kitu fulani mimi sikumbaliani nacho kingekuwa hivi na hivi, na hapo mlele ripoti kama groups ama hata individuals, ulete ripoti hii ya Commission ikitoka kwa coordinator halafu ifike kwa secretariat yetu, haya maoni yote ikifika, itaenda kwa wajumbe wenu amba ni delegates wa National Conference. Mkutano utanza tarehe ishirini na nane October hata ingawa tutawaita mbele hapo kidogo hapo watajulishwa ili watayarishwe kwa agenda na mambo mengine, lakini mtajulishwa commencement of this conference is 28<sup>th</sup> October ili iwe mwezi mmoja kutoka siku ile tuli-launch hii.

Kwa hivyo hayo mambo yenu yote yakija yataenda kwa wajumbe hao delegates. Na watazungumza mambo, watakaa karibu mwezi moja wakiwa na mkutano na wataingilia kila kitu. Haya maoni yenu mnasema yapinduke nini, watayazungumza. Like now we are talking ninajua kuna wengine wameeanza kuzungumza, kutoka tarehe 27 watu walanza kuzungumza kwa sababu tulipeana kwa Kenya yote. Kwa sababu tulisema wacha twende kwa constituencies nayo tuanze. Tungewaachia hivi tu na muendelee kusoma, lakini tukaona ni vizuri Commissioners waende kwa kila Constituency, hii ndio imefanya nije hapa tukiwa na staff, ili tuwaonyeshe ya kwamba hii imeedingia na muendelee kusoma. Kwa hivyo hawa wajumbe wakizungumzia hii na waone kuna mambo wanetaka kugeuza, na kama vile nimewaambia kuna wengi wameaanza kugeuza already wameeanza kuleta proposal ya kusema mimi sisikilizani na hii. Wengine wanaskia mambo ya provincial administration wanasema hiyo ingekuwa namna ingine. Sisi hatuna nguvu ya kugeuza leo, hata ukiniambia hakuna kitu ninaweza kugeuza kwa sababu hii ni proposal ya Commission na hii yenewe itaenda kwa delegates, na ndio wako na nguvu sasa ya kusema kama wategeuza kama watasema hivi. Halafu yale watarecommend, yale yanatengenezwa tena na Commission yawe sawa sawa na baadaye iende kwa Parliament.

Parliament unajua nayo iko na freedom yake ya kuzungumza hata ingawa sijui kama wata (inaudible) na conference kwa sababu hao ni members. Pengine wataendelea vizuri. Conference yenewe inaweza kukataa kukubaliana. Kulingana na sheria ambayo tunayo, inasema kwamba wasiposikizana wanasema wanaweza kupeleka mambo kwa wananchi ambayo tunaita national referendum, na hii ni maoni ya wananchi kutafuta maoni ya watu. Hiyo ingekuwa kuleta kwa nyinyi na mseme vile mnataka mwisho. Lakini hapo tuanona hii conference yetu pengine itatua kila kitu na wamalize lakini wasipomaliza sheria inakubali waendelee tu kwa referendum. But I hope they are going to agree, they come to consensus and may be everything there the matter goes to Parliament.

Sasa tukienda kwa hii kabla ya kuanza kufunga chapter kidogo kidogo, kitu kingine nimebakisha hapa ningetaka kuwajulisha, hii Draft tulipeleka kwa Parliament tarehe 30 sasa ukipatinisha hiyo, utaona Commissioner inaendelea kufanya kazi hiyo kwa utaratibu. 18<sup>th</sup> report kama hii ikatoka, 27<sup>th</sup> September tukaleta Constitution yenewe Draft. 30<sup>th</sup> September tukapeleka hiyo

Draft copy and Draft kwa Parliament, kwa sababu Parliament ndio walichagua Commission, na ni lazima tu-report kwa select committee ya Parliament which is headed by Raila Odinga. Na kutoka hapo sasa, hiyo committee ndio itapeleka sasa kwa Parliament after National Conference.

Sasa tunaenda kwa stages, na unaona siku ya leo tumeweza kufika kwa Constituency, tuko hapa Igembe Constituency kuna wengine wako pahali pengine, kama kesho nitaenda Ntonyiri, kesho kutwa sababu kesho I think ni public holiday. Tarehe kumi na moja tutaenda Rare, kutoka hapo tutaenda upande wa Tigania East, Mikinduri na halafu tumalizie hapo twende mahali pengine. Jana tulikuwa Chuka. Kwa hivyo tunaenda kwa kila Constituency na tukifika huko kama leo mkienda nyumbani ninyi kazi yenu nikuenda kujadiliana ama kutoa makosa ama kuongeza, na ikifika thirty days mlete feedback yenu yaani izungumziwe.

Hebu sasa tuende kwa Draft ambayo ni very important na ndio mtasomo. Kitu cha kwanza ningetaka kuwajulisha mpango moja ambaon mtaona kuna tofauti kidogo na Constitution ya zamani. Katika hii Draft yetu ebu tuingie page ya dani kidogo, page five hivi, hebu tuangalie pahali pamoja kumeandikwa chapter four citizenship. Genereal principles concerning citizenship. Mnaona hii ending ya hii citizenship imeandikwa hapo juu ending, tunaandika hivo, lakini ukiangalia katika Katiba ya zamani ama ambayo tunayo siku hizi. Heading inafanywa na paragraphs. Lakini kwa hii Draft yetu heading imeandikwa huko juu.

Na utaona huyo ndiyo mwendo wake. Kama ukiangalia mahali pengine kama hapo kumeandikwa acquisition of citizenship, utaona pahali pengine imeandikwa languages, the laws of Kenya and so on, na inaandikwa juu. Hii ya zamani ilikuwa ianandikwa kwa paragraphs, yaani kando, upande, wale wamefungua hii pengine wameiona, hiyo utaangalia uone kuna tofauti kidogo. Hiyo haina mambo makubwa, vile unaweza kuandika kitabu useme mpango wangu ni aina hii na mwingine namna hii. Sasa mpango wa Katiba mpya tumekubali iwe juu si upande.

Tukienda kwa page two, uangalie kwa page two, kutoka page two na page three hii ndio inaitwa table of contents ama yale yako ndani ya hii Draft yetu. Kabla ya kuanza kusoma ndani uangalie table of contents ili uchague kile unataka kuzungumza. Utaona hii table of contents ina chapter one, utaangalia hapa chapter one inaanza page two hapo juu na heading yake imeandikwa hapo juu, ‘Sovereignty of the people and the supremacy of the Constitution’ maelezo yameandikwa hapa, na ukienda page 3 utaona mwisho wa chapter. Tuko chapter 20 na utaonaimeishia 299. kwa hivyo hii document iko articles 299 na hapo chapter imefika chapter 20. Ukitaka kuchukua kitu moja ukisome kuhusu hii chukua kwa mfano.

(inaudible) ungetaka kuangalia ni hapo katika arrangement of articles. Table of Contents, Arrangement of Articles, then there is the word Preamble, mnaona hiyo wale wanaojua kusoma, Preamble ni kama utangulizi ama type of introduction. Katika Katiba ambayo tunayo haina Preamble hata ukifungua hapa, hii inaanza tu na may be (inaudible) of Kenya, as it may be prescribed na inaendelea namna hiyo mpaka mwisho na hakuna Preamble. Hii utangulizi ni watu walisema. Hata nkipata nafasi niende through hapa ama kama coordinators (inaudible) ya kusaidia kwa hiyo ya Igembe tutaona ya kwamba watu wa Igembe walisema mambo ya Preamble hapa hapa. Kuna mmoja pengine alisema hiyo? So it is there? Hebu coordinator atafute tukiwa

tunazungumza tutaiona, Igembe walisema tuwe na Preamble hata Ntonyeri walisema. Hii nakumbuka, nilikuwa Igembe nilikuwa Ntonyeri, niienda upande mwingine wa Tigania West na hata wengine walisema.

Okay hebu tuone, watu wa Igembe waliongea mambo ya Preamble. ‘The Preamble should state that Kenya is a God fearing country’ mtu mmoja alisema. Mwingine alisema the Preamble should state that no Kenyan should be above the Constitution the Preamble should capture Kenyans historical background the. Preamble should express the sovereignty of all Kenyans. Kwa hivyo hapa kuna mapendekezo mengi yale ulisema iwekwe kwa Preamble, kwa sababu tuliona hayo mari-recommendation kutoka kila mahali 210 constituencies then we made a summary ambayo inacapture ati kuwe na Preamble. Kwa hivyo hata Igembe Constituency ilisema tuwe na utangulizi na kama nikisema nisome saa hii, utaona wale walikuwa wakisema historical background, there is an arrangement there. God fearing people, utaona kuna kitu kama hicho. Na hicho kilisemwa hapa hapa. Kwa hivyo mnaona ni maoni yenu, It’s a people driven Constitution. Tumetoa maoni ya Igembe tumetoa kila pahali kwa wananchi.

Hebu tujaribu kusoma Preamble tuone yaani utangulizi wa hii Katiba mpya ambayo itatoka

“ We the people of Kenya are aware of our ethnicity, cultural and religious diversity and determine to leave in peace and unity as one sovereign nation committed to nurturing and protecting the well being of the individual, the family, and the community within the nation. We recognize aspirations for our women and men and a Government based on the essential values of freedom, democracy, social justice and the rule of law, exercising our sovereign and inalienable right to determine the form of governors of our country and having fully participated in the Constitution making process, do adopt, enact and give to ourselves and to our future generations this constitution. God bless Kenya.

Unaona mambo yako ndani ndani yale yale tu watu wamependekeza, huu ni utangulizi na utaendelea kusoma yale mambo yamewekwa kwa hii Draft yote. Kwa sababu nawaonyesha vile table iko, ukiona kitu fulani na unataka kujua ni kitu gani, let me take an example here. Chapter two the Republic, hebu tuchukue article number nine kwa mfano, languages, tuone Draft inasemaje kwa Draft. Ukienda number nine nitaanza page four, wengine mmeputa now languages imesema hivi, the official languages of Kenya are Kiswahili and English and all official documents shall be made available in both languages. Sasa ni watu wenyewe walisema hivyo.

Tukiangalia Igembe Constituency tutaona pahali ambao watu wamesema Kiswahili kiwe official language. Ile imekuwa official language in Kenya mpaka leo ni English, Kiswahili is just a national language, tuanita nationala yaani ya kuzungumzwa na kila mtu. Lakini kuingia kwa vitabu vya Serikali katika law huwezi kuona Kiswahili huko. Lakini kwa hii Katiba mpya tunataka kuwe English na Kiswahili. Wakati hii Katiba itakuwa tayari kwa hizo stages zote ikienda through, wakati huo sijui itakuwa page ngapi kwa sababu inaweza kuongezewa kidogo ama kufupishwa lakini kama hii ya sasa unaona iko na pages 98, pengine inaweza kuwa zaidi kidogo. Lakini itakuwa kitabu kama hiki na kitakuwa kitabu cha sheria ambacho kimeenda all through these stages. Lakini unajua kilitengenezwa na mzungu na Serikali ya Kenya ilianza kui-review mpaka ikawa vile ilivyo, tukasema

ibadilishwe kidogo. Sasa hii yetu itakuwa kitabu kama hiki, sasa itakuwa kwa Kiswahili na Kiingereza. Kwa hivyo official language inamaanisha ni luga ya maofisi ya kutumia kwa ofisi.

Hapo number two yake inasema ya kwamba the national language of Kenya is Kiswahili kwa hivyo Kiswahili it is going to be official at the same it will continue to be our national language. May be a certain time will come in future, watu wetu wanaweza kufikiria waseme hebu tufanye Kiswahili official peke yake. Lakini wakati huu tunesema iwe national language pamoja na English. Kama Tanzania Kiswahili is the official language. Ukienda huko Kiswahili, wale wanazungumza lugha zingine, lakini Kiswahili ni official and national. Sasa tunasema tumekubalia mpaka sasa kiwe official na national lakini inaenda na ingine, we cannot change at once, lazima ziende pamoja. All the same inategemea ikienda kwa national conference hawa wajumbe wenu wakienda wakiona ya kwamba iwe official language na waondoe kiingereza hiyo pengine itakuwa mamlaka yao, na unajua Commissioners hawatapiga kura wataachia hao ndio wakubwa kabisa ndio wanaweza kugeuza ama kuongeza kwa hii.

Hata ninyi wenyewe makiona kuna kitu mnalalamika mna kitu mnataka kuondoa au kuongeza, we have given you this one to read for thirty days. Sasa hiyo ni mfano nimewapatia mwengine wa kusoma. We can get another example, (interjection).....

Now twende kwa sehemu ingine ningetaka tuangalie sisi zote, Legislature page 13, this is at the bottom, utaona chapter seven page 13 part one. Legislature ni ile group inafanya sheri, na ya kwanza hapa ni Parliament part one. Establishment of Parliament: there shall be a Parliament of Kenya (I am reading page fourteen on top), we shall consist of the national council and the national assembly. So the Parliament will have two chambers, what we used to call upper house and the lower house, sasa unafikiria ni Commissioners walipendekeza hiyo? Ni wananchi, na hapo nilikuwa nikisoma na ninaweza kuwasomea vile watu wa Igembe walisema vile tuko hapa kuhusu hiyo. Watu wa Igembe nasoma vile watu wa Igembe walisema hapa hapa tuko kuhusu hiyo, kuna mtu alisema, "the Constitution should provide for a bi-cameral Parliament with an upper house of elected Mps with an Upper house," si unaona Igembe ilisema? Sasa mambo ya Igembe na ya wapi 210 of them tuliweka pamoja, and we provided for two chambers of Parliament. Watu hapa walikuwa wakisema iitwe lower house na ingine upper house. Unajua ilikuwa hapa zamani ilikuwa tunaita upper na ingine lower house hata ilikuwa inaitwa senate na ingine inaitwa house of representatives na yote ilikuwa inaitwa National Assembly, lakini sasa unaona vile mpango ilivyo tumechukua maoni ya watu ya watu kwa sababu hata ukisoma hapa huyu ni mtu mmoja amesema hivyo lakini kuna mwengine anasema hivyo hivyo kwa lugha nyininge.

The Constitution should provide for a two chamber of Parliament, yule mwengine alikuwa anaita bi-cameral Parliament. Hiyo ni kimombo ya kuonyesha hata hiyo ni kusema nyumba mbili lakini mwengine straight away there should be a two chamber of Parliament so he has become simpler and this away we have tried also to simplify the language, anasema just the same thing.

The upper house should comprise five members from each of the country's provinces and should be charged with the duty of supervising the President. Hiyo ni maoni tu ya mtu fulani, lakini the main thing is he is recommending two houses. The

Constitution should provide for a two chamber of Parliament. The upper house should have a veto power over the lower house, hiyo ni kazi sasa ya upper house. So the thing is that you recommended that one na mliongea sana, mlipeana hiyo maoni ya 2 houses yameandikwa maoni mengi ya watu tofauti hapa. Sasa hayo maoni tuliyapata kila Constituency katika Kenya and on putting down in brief the actual recommendations that is where we say, depending on what we heard from the people there shall be a Parliament of Kenya which shall consists of two houses the National Council and the National Assembly.

For us we decided to name these houses National Assembly ambayo ni ya house of representatives which we call lower house, na ile ya juu tukasema tuite jina National Council. Hayo ni majina tu hiyo ndiyo wengine wanaita senate kama America ama pahali pengine. Hata Kenya tulipoanza 1963 ilikuwa inaitwa senate sasa tumechukua maoni ya wananchi wanataka two houses but we preferred the name National Council, for the upper house and for the lower house National Assembly. So those two houses make Parliament.

The law of Parliament niliwaambia kwamba hatutasoma hiki kitabu chote lakini nawapatia guideline ya kuweza kusoma kwa njia mzuri by way of launching. Utaangalia for only role of Parliament ile kumbwa sana ni kufanya sheria. Hii upper house pahali pamoja utaona impeachment of President ndio itakuwa inafanyiwa sana. Kama kitu kama approving of international treaties hata hiyo ni Parliament, approving declaration of emergency and war it is also Parliament. Parliament shall protect this Constitution and promote the democratic governors of the republic. So you go through as you continue reading for thirty days, you go through many times there you see the law.

Approval of appointments by Parliament, that is also a very important point, kitu cha muhimu sana kwa Parliament kufanya hiyo kwa sababu (inaudible) haikuwa ina approve hapo mbeleni. Lakini sasa lazima Parliament iidhinishe appointment ama kuchagua wafanyi kazi wa Serikali. Pengine wale wa juu sana kama PS ama tumeona Ministers, Ministers watachaguliwa na Parliament kwa sababu si MPs kulingana na our recommendation, na hii recommendation ilitoka kwenu. Watu walisema hayo kutoka kila Constituency, kwa hivyo approval of Parliament kama ukiendelea kusoma hapa utaona watakuwa wana-approve kama ni Commissions, utaona list ya Commissions judicial service Commission, ethics and intergrate Commission, land and national land Commission, hii ningetaka kuwaeleza ni kitu mpya kabisa na hii tunahusika sana sisi wote wananchi wakulima ama wananchi wa Kenya kwa sababu ya mashamba ndio ya muhimu sana.

National Land Commission, tuliangalia mambo ya mashamba malalamiko yote kutoka coast kutoka wapi Kenya yote na tukaona lazima kuwe na Commission ambayo itaangalia mambo ya mashamba, haikuwako mbeleni. Mbeleni ilikuwa tu inaitwa Commissioner of lands huyo ni mtu mmoja lakini ana ofisi yake one person Commission, na mtu mmoja ana makarani wake wanaweza kufanya mambo mengi mambaya yale wanataka, but this one is going to be a Commission. Yaani itakuwa Commission sasa ya watu wengi na Parliament itaonyesha vile watachaguliwa. Hii Commission ndio itakuwa inasema kitu fulani inapeleka Bunge inasema kama ni mambo ya law, laws za mashamba kama hii inasumbua watu sana inaitwa Cap 283 hii ya consolidation, hii inatoa mtu hapa inapeleka huko katika mlima, majani yake inapotea, kahawa na nini, kama hiyo Commission

hii ita-change kama hiyo.

Laws zingine za kuandikisha mashamba wataona ile mbaya mbaya wa-change. Kwa sababu tuna law nyingi inahusu mashamba mengi sana na hizo zote zitawekwa pengine ziwe kitu kimoja, iwe law kama mbili tatu ya registration na pengine iwekwe ya kuangalia mambo ya mashamba yote. Kwa hivyo hiyo land Commission ni kitu kimoja tumetokea nacho katika Draft hii ya Constitution na tuliamiwi na watu, kuwa na ministries si ministries peke yake lakini Commission. Ministry inakuwako lakini Commission itaingilia ndani ndani zaidi mpaka itekeleze yale mambo watu wanakubali, na hii itachaguliwa haraka sana. yaani Serikali ikianza, wajumbe wakipatikana (inaudible) na nini, kitu cha kwanza ni kuanza Land Commission, Constitutional Commission, kama Public Service Commission, Judicial Commission, yaani watengeneze hizi Commission zote nazo ziendelee na kazi.

Hebu niangalie hapa members of the national council, this is Act 106, elections for the National Council shall be held:

A. For seventy members on the bases of single member constituencies and (inaudible) for women candidates and multinumber Constituency representing provinces and Nairobi. Vile kutakuwa hapa ni kwamba tumekubali constituencies are (inaudible) itakuwa district, the current districts, sasa tuko na 69 districts. Kutoka hii Meru North, Meru Central mpaka South zote ni 69. Kwa hivyo kutakuwa na mmoja mmoja kutoka kwa kila district kwa hiyo house ama National Council. Sasa hawa watakuwa 69 na mmoja atatoka Nairobi kwa sababu Nairobi itachukuliwa kama district kwa yule mpango umepangwa wa devolution of powers, itakuwa kama district sasa wamekuwa ngapi, si seventy? Nao wao wamebaki thirty ili wafanye hundred watakuwa akina mama nao watatoka kwa provinces kila province wanne, na tuna province ngapi? Provinces?

**Audience:** (inaudible)

**Com Ratanya:** There are seven na pamoja na Nairobi eight. Sasa seven kila moja itatoka wanne hao ni wangapi kwa mahesabu? Na fanya hesabu ile ya Kerry Francis ya haraka haraka.

**Audience:** Twenty eight

**Com Ratanya:** Twenty eight, Nairobi watachaguliwa wawili watakuwa wangapi? Thirty. Sasa ukiunganisha na wale seventy ni wangapi?

**Audience:** Mia moja.

**Com Ratanya:** Mia moja yaani watakuwa na one hundred members kwa National Council, hii ambayo mmejua ndio tunaita upper house lakini the official name proposed here is the National Council.

Hebu tuendelee hapa for the purposes of elections under clause one A, Constitution shall be based on districts including

Nairobi. This I have said already you will read there for the purpose of election under one B, (inaudible) as follows four women representing each of the provinces and two women representing Nairobi, I have told you that, nitasoma zaidi. In the elections under clause 3, every voter may vote for only one candidate and the candidates in the case of provincial seats who are among the four top are in the case of Nairobi seats the two candidates shall be elected, hawa wote tunaona sasa wamefanya National Council.

Twende kwa National Assembly, National Assembly ni lower house or house of representatives. Mnajua hawa members wanatoka kwa constituencies, simply kama sasa tuna 210 katika National Assembly, hao wataendelea kuwa 210 namna hiyo mpaka wakati constituencies zitakuwa revised na kutakuwa na process na revision of constituencies in future. This Draft has provided that somewhere, lakini leo tuna 210, kwa hivyo kutakuwa na 210 members of the National Assembly according to our proposal here in this Draft. Tumependekeza kuwe na wengine ninety ambao pia watakuwa kwa National Assembly na hao ninety watawafanya wale wengine wawe 300, kwa hivyo National Assembly, itakuwa 300 members, na National Council 100 members.

Njia ya kuchagua hawa ninety, hawa wanapendekezwa ili wa - represent marginalized groups kama akina mama, disabled na wengine, lakini Parliament wakati mambo hii itanza for implementation kutakuwa na guidelines za kuonyesha vile watachaguliwa.

Ukienda kwa qualifications hakuna maneno mengi sana kwa qualifications hapa ni 108, qualifications and disqualification of members, hapa mtasoma. Mtaona kitu cha muhimu sana ni kuwa mwananchi wa Kenya a citizen of Kenya. You can see other qualifications like attaining the age of 35 in the case of National Council, shall attain the age of 21 in the case of National Assembly. Sasa hapo yote utaangalia na utaona hata disqualifications kama mtu akiwa of unsound mind, akiwa is bankrupt, yaani mtu akiwa bankrupt. Hiyo point ya bankrupt watu wengi wanasema kama kule luhya, lakini sijui hata hapa pengine mtu alisema. Ya kwamba tukifungia hawa watu maskini hawatapata viti hata ikiwa ni kiongozi. Kwa sababu yule mtu anaitwa bankrupt ni yule amekuwa maskini kabisa amefirisika hata hawezi kulipa deni. *Kana tiguo?* Namna hiyo. Sasa kuna watu walikuwa wanauliza, tukiweka hiyo kwa Katiba haitafungia maskini? Kwa sababu ye ye amefilisika amekuwa maskini, watu wengi waliuliza hivyo walikuwa wanasema hiyo tusiweke. Lakini wengi nao walikuwa wanasema mtu akiwa ni maskini hata chakula hawezi kupata, hata hawezi kulipa deni huyo hawezi kuongoza. Mnajua hata kwa kienyeji mtu ambaye hana kitu chochote alikuwa kweli anaenda mbele ya watu sana? Yaani (**vernacular**)

**Audience:** (Inaudible)

